



اموال ہیرے (Swahili)

# ALMASI ZENYE THAMANI KUBWA MNO



Sheikh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat  
Muasisi wa Dawat-e-Islami, Ailamah Maulana Abu Bilal  
**MUHAMMAD ILYAS**  
Attar Qadiri Razavi



آمول ہیرے

Anmol Heeray

# Almasi zenye thamani kubwa mno

Kijitabu hiki kiliandikwa na Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Aḥl-e-Sunnat, muanzilishi wa Dawat- e-islami ‘Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دامت بركاتهم العالیة Katika lugha ya Kiurdu. Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Majlise Tarajim. Endapo utaona makosa yoyote katika tafsiri yake au utungaji wake, tafadhali wajulishe Majlise Tarajim kwa njia ya posta au kwa kipepesi ili upate thawabu.

## Majlis-e-Tarajim (Dawat-e-Islami)

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran,  
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

UAN: ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 1262

Email: ✉ translation@dawateislami.net

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ  
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo.  
Insha-Allah عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللَّهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَاَنْشُرْ  
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Ee mola عَزَّوَجَلَّ Ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie mtakatifu kabisa.

*(Al-Mustatraf, vol. I, pp. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)*

**Kumbuka:** Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na baada ya dua.

## Table of Contents

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu .....	ii
<b>Almasi zenye thamani kubwa mno .....</b>	<b>1</b>
Ubora wa kumsalia Mtume ﷺ .....	1
Maisha ni almasi yenye thamani kubwa.....	2
Maisha ni mafupi.....	3
Ushanga wa pumzi .....	4
Siku hunadi.....	5
Bwana au marehemu.....	5
Kifo huja ghafla.....	5
Majuto hata Peponi .....	6
Nibu ya kalamu.....	6
Fanya upandiwe mti Peponi .....	7
Ubora wa kumsalia Mtume.....	7
Ni bora kuliko miaka 60 ya ibada.....	8
Mambo 5 kabla ya 5 .....	9
Neema 2 .....	9
Uzuri wa Uislamu.....	10
Kuthamini wakati wenye faida kubwa.....	10
Kauli za wanaothamini wakati.....	10
Panga ratiba.....	12
Fadhila ya asubuhi.....	14
Maua 15 ya hekima kuhusu kulala na kuamka .....	15

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ  
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

# Almasi zenye thamani kubwa mno\*



Shetani atatumia kila hila ili kukuzuia kusoma kitabu hiki, lakini utangiwa na hofu ya Allah عَزَّوَجَلَّ kubwa baada ya kukisoma  
إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ.

## Ubora wa kumsalia Mtume ﷺ

A'lā Ḥaḍrat Imām-e-Ahl-e-Sunnat Maulānā Shāh Imām Aḥmad Razā Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ الرَّحْمَنِ ametaja katika Fatāwā-e-Razaviyyah, Juz. 23, uk. 122: Sayyidunā Abul Mawāhib رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema: Nilimwona Mtume Kipenzi Mwenye Rehema صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ katika ndoto. Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akaniambia, 'Utawaombea msamaha watu laki moja Siku ya Kiama.' Nikauliza, 'Ewe Mtume! Nilipata vipi hadhi kubwa kama hiyo?' Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

---

\* Bayana hii ilitolewa katika ijtimai ya siku 3 ya sunna ya Dawat-e-Islami, Şehrâ-e-Madinah, Bâb-ul-Madinah, Karachi tarehe 25 Şafar-ul-Muzaffar, 1430.

akasema, ‘Kwa sababu unanalisalia kisha unanifikishia thawabu za sala ulizonisalia.’ (*Al-Ṭabqāt-tul-Kubrā lish-Sha’rānī, uk. 101*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Ili kufikisha thawabu, tia nia ya kufikisha thawabu moyoni huku unamsalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ama sema kabla au baada ya kumsalia, ‘Nanuilia thawabu hizi za kumsalia Mtume zimfikie Kipenzi Mtume Inaezwa kuwa, siku moja mfalme na wenzake walipita kwenye shamba la matunda. Wakamwona mtu anarusha vijiwe; kijiwe kimoja kikampiga mfalme. Mfalme akaamrisha wafanyikazi wake wamshike na wamlete mtu yule kwake. Basi mtu yule akapelekwa kwa mfalme.

Mfalme akauliza, ‘Vijiwe hivi umevipata wapi?’ Mtu yule aliyekuwa na hofu akajibu, ‘Niliviona vijiwe hivi nilipokuwa nikizurura msituni, nikavitia mfukoni mwangu. Nilipofika katika shamba hili nikavitumia kupuria matunda.’ Mfalme akauliza, ‘Je, unajua thamani ya vijiwe hivi?’ Akajibu, ‘La.’ Mfalme akasema, ‘Vijiwe hivi vidogo ambavyo umevitupa kwa ujinga wako ni almasi zenye thamani kubwa mno.’ Aliposikia hayo, alijuta, lakini ifalieni ili hali alikuwa ameshapoteza almasi zenye thamani kubwa kabisa.

## Maisha ni almasi yenye thamani kubwa

Ndugu waislamu! Maisha ni sawa na almasi yenye thamani kubwa. Tukiyapoteza kwa mambo ya kipuuzi, hatutapata chochote ila huzuni na majuto Siku ya Kiama.

Allah عَزَّوَجَلَّ amewaleta wanadamu duniani kwa muda mfupi ili kutimiza malengo maalum. Kwa hivyo, imetajwa katika Sūrah Muminūn, ayat 115:

أَحْسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ ﴿١١٥﴾

***Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?***

*[Kanz-ul-Īmān (Tafsiri ya Quran)] (Parah 18, Sūrah Muminūn, Ayat 115)*

Imeandikwa katika Khazāin-ul-‘Irfān kuhusu aya hii: ‘na (mlidhani) kwamba hamutafufuliwa ahera kupata malipo yenu! Bali nimewaumba kwa ajili ya ibada ili nilazimishe juu yenu ibada na kesho ahera murudi kwangu niwalipe malipo ya matendo yenu.’ Maelezo kuhusu lengo la uhai na mauti, imetajwa katika Surah-tul-Mulk, ayat 2:

الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۗ

***Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi.***

*[Kanz-ul-Īmān (Tafsiri ya Quran)] (Parah 29, Surah-tul-Mulk, Ayat 2)*

## **Maisha ni mafupi**

Ndugu waislamu! Lengo la maisha limeelezwa katika ayat

zingine mbali na aya hizi mbili. Mwanadamu ataishi katika ulimwengu huu kwa muda mfupi. Katika muda huu mfupi, lazima ajitayarishe kwa ajili ya muda mrefu mno wa kaburini na Siku ya Kiyama. Kwa hivyo muda tulionao sasa ni muhimu mno. Wakati hupita haraka na hauwezi kudhibitiwa wala kusimamishwa. Pumzi zilizoachiwa haziregei.

## Ushanga wa pumzi

Sayyidunā Ḥasan Baṣrī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alikuwa akisema, ‘Harakisha, Harakisha! Ukweli wa maisha yako ni nini-maisha yako ni pumzi chache tu. Zikisimama, amali zako zinazokupatia radhi za Allah عَزَّوَجَلَّ pia zitakoma. Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ kuwa na rehema juu ya mtu ambaye anajihisibu na hutokwa na machozi anapokumbuka dhambi zake!’ Kusema hivyo, Yeye رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alisoma aya 84 ya Suratul Maryam:

إِنَّمَا نَعُدُّ لَهُمْ عَدًّا ۗ

*Sisi tunawahisabia idadi ya siku zao.\**

*(Kanzul Īmān [Tafsiri ya Quran])*

Ḥujja-tul-Islām Sayyidunā Imām Muhammad bin Muhammad Ghazālī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى الْوَالِي amesema, ‘Hesabu inarejelea idadi ya (mpumuo wa) pumzi.’ (*Iḥyā-ul-‘Ulūm*, juz. 4, uk. 205)

---

\* Siku zilizosalia kwao au matendo yao maovu.



## Siku hunadi...

Sayyidunā Imām Bayḥaqī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِيّ ameandika katika Shu'ab-ul-Īmān: Mtume mwenye rehema, صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, 'Kila siku jua linapokuchwa, siku hunadi 'ikiwa unataka kutenda amali njema leo, basi tenda kwa sababu sitarudi tena.'

*(Shu'ab-ul-Īmān, juz. 3, uk. 386, hadithi 3840, Dar-ul-Kutub-ul-Ilmīyah, Beirut)*

## Bwana au marehemu

Ndugu waislamu! Tufanye amali njema kwa wingi tuwezavyo ili tufaidike na uhai kwani huenda tukafikwa na kifo wakati wowote. Wanaotuita 'Bwana' leo huenda wakatuita kesho 'Marehemu'. Bila shaka tunakimbilia kifo kwa haraka ingawa hatutanabahi. Inaelezwa katika suratul Inshiqāq, aya 6:

يَا أَيُّهَا الْإِنْسَانُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَدًّا مَّا مَلَقَيْهِ ۗ

*Ewe mtu! Hakika wewe unajikusuru kwa juhudi kumwendea Mola wako Mlezi, utamkuta.*

*[Kanz-ul-Īmān (Tafsiri ya Quran)] (Parah 30, Surah-tul-Inshiqāq, Ayat 6)*

## Kifo huja ghafla

Enyi munaopoteza muda wenu katika mambo ya upuuzi! Zingatieni kwa makini. Uhai wetu unamalizika haraka. Mara nyingi mutakuwa mumewahi kuona mtu mzima akifa ghafla; hatujui kuhusu hali yake kaburini lakini yeye ashatambua hali ya maisha yake.

Enyi munaotamani utajiri wa duniani! Enyi munaozingatia ujilimbikizaji mali kuwa ndilo lengo la pekee la maisha! Fanyeni haraka na jitayarisheni kwa maisha ya baadaye musije mukalala usiku salama afya zenu na asubuhi ikawa mumelazwa kaburini. Nawaombeni kwa ajili ya Allah! Muzinduke kutoka kwenye usingizi wa mughafala. Allah عَزَّوَجَلَّ amesema katika Sūrah Anbiyā:

اِقْتَرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ مُّعْرِضُونَ ﴿١﴾

*Imewakaribia watu hisabu yao, nao wamo katika mghafala, wanapuuzua . [Kanz-ul-Īmān (Tafsiri ya Quran)] (Sūrah Anbiyā, ayat 1)*

## Majuto hata Peponi

Ndugu waislamu! Ni muhimu kuthamini wakati. Kupoteza wakati kwa mambo ya kipuuzi ni hasara kubwa. Kama alivyosema Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, ‘Watu wa Peponi hawatajutia chochote duniani ila ule muda ambao hawakuutumia kumkum buka Allah عَزَّوَجَلَّ.’ (Mu’jam Kabīr, juz. 20, uk. 93-94, Ḥadīthi 172, Dārā-hayā-ul-Turāṣ, Al-‘Arbī, Beirut)

## Nibu ya kalamu

Hāfīz Ibn ‘Asākir ameandika katika Tabyīn-u-Kazīb-il-Muftarī: Kalamu ya Sayyidunā Salīm Rāzī رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ (mwanachuoni mkubwa wa karne ya 5) ilipomalizika kwa ajili ya kutumika

sana, yeye رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ angetaja Allah عَزَّ وَجَلَّ halafu angechonga kalamu yake (Huku ni kuua ndege wawili kwa jiwe moja kwani kuandika kwa ajili ya dini ni thawabu). Angetumia wakati wake vizuri.

## Fanya upandiwe mti Peponi

Kwa sekunde moja mtu anaweza akafanya apandiwe mti Peponi kwa kutumia wakati vizuri. Njia ya kufanya upandiwe mti Peponi ni rahisi mno kama alivyoeleza Ibn-e-Mājah katika hadithi, ‘Atakayetamka moja kati ya maneno manne haya atapandiwa mti Peponi’. (1) سُبْحَانَ اللَّهِ (2) الْحَمْدُ لِلَّهِ (3) لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ (4) اللَّهُ أَكْبَرُ. (Sunan Ibn-e-Mājah, juz. 4, uk. 252, Hadithi 3807)

## Ubora wa kumsalia Mtume

Ndugu waislamu! Tazama ilivyorahisi kupandiwa mti Peponi! Mtu akitaja moja ya hayo, atapandiwa mti; akitaja yote manne basi miti minne atapandiwa Peponi. Kwa hivyo tanabahi umuhimu wa wakati; miti hupandwa kwa ajili yetu kwa sababu ya kutamka maneno machache tu.

Badala ya kupoteza muda katika maneno ya kipuuzi tungejipandia miti isiyohisabika Peponi kwa kuleta uradi wa ‘سُبْحَانَ اللَّهِ سُبْحَانَ اللَّهِ’. Tuwe tumesimama, tumekaa au tunafanya kazi tumsalie Mtume kwa wingi kwa sababu malipo yake ni makubwa mno. Mtume Kipenzi aliyebarikwa صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

amesema, ‘Anayenisalia mara moja, Allah ﷺ humteremshia rehema 10, humsamehe madhambi 10 na humpandisha daraja 10.’

*(Sunan Nasāī, uk. 222, Ḥadithi 1294, Dār-ul-Kutub, Beirut)*

**Kumbuka!** Unaposoma uradi ukiwa umejinyosha basi (ni katika adabu) ukunje miguu yako.

Ndugu waislamu! Tungefanya mazoea ya kuwa wazingativu kabla ya kuzungumza iwapo tunachotaka kuzungumza kina faida ya kilimwengu au ya ahera. Ikiwa hakina faida, tumsalie Mtume au tuanze kumtaja Allah ﷺ badala ya kujiingiza katika mazungumzo ya kipuuzi ili tupate thawabu. Tusome: ‘سُبْحَانَ اللَّهِ’, ‘الْحَمْدُ لِلَّهِ’, ‘لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ’, ya ‘اللَّهُ أَكْبَرُ’ ili tupandiwe miti Peponi.

## Ni bora kuliko miaka 60 ya ibada

Ikiwa hutaki kusoma chochote, ukinyamaza pia unaweza kupata thawabu. Badala ya kufikiria mambo ya kidunia ya kipuuzi, mkumbuke Allah ﷺ na Mtume wake صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Tafakari kuhusu elimu ya dini au adhabu ya kifo, upweke wa kaburini na vitisho vya Siku ya Kiama. Wakati wako hautapotea bure na kila pumzi إِنَّ شَاءَ اللهُ ﷺ ihisabiwe ni ibada. Imetajwa katika Jāmi’-uṣ-Ṣaghīr kuwa Mtume Kipenzi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘Kutafakari (juu ya ahera) kwa muda ni bora kuliko miaka 60 ya ibada.’

*(Al-Jāmi’-uṣ-Ṣaghīr, uk. 365, Ḥadithi 5897, Dār-ul-Kutub Ilmīyah, Beirut)*

## Mambo 5 kabla ya 5

Ndugu waislamu! Hakika maisha ni mafupi. Kwa kweli muda uliopo ndio ulionao, matarajio ya kuwa na wakati siku zijazo ni uongo. Inawezekana kufikiwa na kifo muda wowote. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ:

إِغْتَنِمَ حَمْسًا قَبْلَ حَمْسٍ: شَبَابَكَ قَبْلَ هَرَمِكَ وَصِحَّتَكَ قَبْلَ سَقَمِكَ  
وَغِنَاكَ قَبْلَ فَقْرِكَ وَفَرَاغَكَ قَبْلَ شُغْلِكَ وَحَيَاتَكَ قَبْلَ مَوْتِكَ

Yapatilize (mambo) matano kabla ya (mambo mengine) matano: (1) ujana kabla ya uzee, (2) uzima kabla ya ugonjwa, (3) utajiri kabla ya ufukara, (4) faragha kabla ya shughuli (5) uhai kabla ya kifo. (*Al-Mustadrak, juz. 5, uk. 435, Ḥadithi 7916, Dār-ul-M'arifat, Beirut*)

## Neema 2

Amesema Mtume wa ulimwengu, Amani ya moyo, na Karimu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ‘Watu hudanganyika na neema 2: uzima na wasaa (faragha).’ (*Ṣaḥīḥ Bukhārī, juz. 4, uk. 222, Ḥadithi 6412, Dār-ul-Kutub Ilmīyah, Beirut*)

Ndugu waislamu! Mgonjwa hugundua thamani ya uzima zaidi kuliko mtu mzima na mtu mwenye harakati nyingi mno anatambua umuhimu wa wakati. Wenye wasaa mwingi kawaida hawaelewi thamani ya wakati. Thamini wakati wako na ujizue kuzungumza upuuzi, matendo yasiyofaa na marafiki wasio na maana.

## Uzuri wa Uislamu

Imetajwa katika Tirmizi Sharif: Rehema ya ulimwengu, Mtume mwenye cheo zaidi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, '(Mtu) kujitenga na matendo yasiyomuhusu ni moja wapo ya uzuri wa uislamu wake.' (*Jāmi' Tirmizī, juz. 4, uk. 142, Hadithi 2344, Dār-ul-Fikr, Beirut*)

## Kuthamini wakati wenye faida kubwa

Ndugu waislamu! Siku za maisha ni masaa na masaa ni sekunde. Kila mpumuo ni almasi yenye thamani kubwa mno. Tungethamini kila mpumuo na kutumia wakati kufanya matendo mema! Tusingelia kwa majuto Siku ya Hesabu tutakapona kitabu chetu hakina kitu chema. Wajibika na zingatia namna unavyotumia wakati wako. Jitahidi kutumia kila muda wa uhai wako katika kutenda mema. Jizuie kupoteza wakati kwa kufanya dhihaka na upuuzi; la sivyo tutakuja kujuta Siku ya Kiama.

## Kauli za wanaothamini wakati

1. Amīr-ul-Muminīn, Sayyidunā 'Alī كَتَمَهُ اللهُ تَعَالَى وَجْهَهُ الْكَرِيمِ amesema, 'Hizi siku ni kurasa za maisha yako, zipambe kwa amali njema.'
2. Sayyidunā 'Abdullāh Ibn Mas'ūd رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema, 'Nahuzunika na naona aibu kwa siku ambayo nimeitumia bila kuongeza amali njema.'

3. Sayyidunā ‘Umar bin ‘Abd-ul-‘Azīz رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema, ‘Kila siku maisha yako yanapungua, mbona bado unaende lea kufanya uvivu kutenda amali njema!’ Siku moja mtu alimuuliza, ‘Ewe Amīr-ul-Muminin! Ahirisha kazi hii mpaka kesho.’ رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ akasema, ‘Simalizi kazi ya siku kwa siku moja; nikiahirisha kazi ya leo hadi kesho, nitawezaje kukamilisha kazi ya siku mbili kwa siku moja?’
4. Amesema Sayyidunā Ḥasan Baṣrī رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ, ‘Ewe mwanadamu! Maisha yako yamejengwa kwa siku. Siku moja ikipita, basi sehemu ya maisha yako pia imepita.’  
*(Tabqāt-ul Kubrā lil Manāwī, juz. 1, uk. 259, Dār Ṣadr, Beirut)*
5. Amesema Sayyidunā Imām Shāfi’ī رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ, ‘Nilikaa na watu wacha Mungu kwa muda fulani nikafaidika kiroho. Nimejifunza mambo makuu mawili kutokana na kuwa nao: (1) wakati ni upanga, ukate kwa amali njema la sivyo utakukata (kwa kukushughulisha na mambo yasiyokuwa na maana) na (2) hifadhi nafsi yako; ikiwa hujishughulishi na amali njema itakushughulisha na mambo mabaya.’
6. Amesema imām Rāzī رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ, ‘Ninaapa kwa Allah عَزَّوَجَلَّ mimi huhuzunika majira ya kula kwa sababu hunibidi niache shughuli za kidini (kuandika au kutwalii). Wakati ni rasilimali kubwa mno.’

7. Hāfiẓ Ibn Ḥajar رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى aliandika kuhusu Sayyidunā Shams-ud-Dīn Aṣbahānī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى (mwanachuoni mkubwa wa karne ya 8 wa kishafi): رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى alikuwa akila kidogo kutokana na hofu ya kupoteza wakati kwenda chooni mara kwa mara. (*Ad Dar-ul-Kalimah ‘Asqalānī, juz. 4, uk. 328, Dār Aḥayā-ul-Turāš Al-‘Arbī, Beirut*)
8. ‘Allāmah Ḥāhbi رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى aliandika katika Taẓkira-tul-Ḥuffāz ya kwamba Khaṭīb-e-Baghdādī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى angetwalii hata akiwa anatembea (ili asipoteze wakati anapokwenda mahali pamoja hadi kwengine). (*Taẓkirah-ul-Ḥuffāz, juz. 3, uk. 224, Dār-ul-Kutub Ilmīyah, Beirut*)
9. Sayyidunā Junaid Baghdādī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى alikuwa akisoma Quran Tukufu wakati wa kifo chake. Mtu mmoja akauliza kwa mshangao, ‘Kusoma (Quran) hata majira haya!’ رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى akajibu, ‘Kitabu changu cha hesabu kitafungwa kwa hivyo ninajitahidi upesi upesi kuongeza amali njema.’ (*Ṣīd-ul-Khāṭir Ibn-ul-Jawzī, uk. 227, Maktabah nazar Muṣṭafā-ul-Bāz*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

## Panga ratiba

Ndugu muislamu! Ikiwezekana panga ratiba ya kila siku. Kwanza, jitahidi kulala ndani ya masaa mawili baada ya sala ya ishai. Ni hasara kubwa kupiga domo na kusengenya (ikiwa hakuna tija ya kidini) hotelini au mahali kwengine. Imeelezwa katika Tafsīr



Rūḥ-ul-Bayān, juz. 4, uk. 166, ‘Sababu moja ya kuangamizwa kwa taifa la Lūṭ ni kwa sababu walikuwa wakikaa kando ya barabara kucheka na kuwafanyia watu dhihaka.

Ndugu waislamu! Hata marafiki zako wakawa wanaonekana kuwa wacha Mungu namna gani, epuke vikao vyao vya kughafilisha watu na kumuudhi Allah عَزَّوَجَلَّ. Lala mapema baada ya kukamilisha ibada za usiku kwa sababu mapumziko ya usiku ni bora kwa afya. Imetajwa katika Sūrah Qaṣaṣ, aya 73:

وَمِنْ رَحْمَتِهِ جَعَلَ لَكُمْ الَّيْلَ وَالنَّهَارَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٧٣﴾

*Na ni katika rehemu zake, amekufanyieni usiku na mchana mupate kupumzika humo na mtafute fadhila zake na ili mpate kushukuru. [Kanz-ul-Īmān (Tafsiri ya Quran)] (Sūrah Qaṣaṣ, ayat 73)*

Katika kushereheshea aya hii, Ḥakīm-ul-Ummat Muftī Aḥmad Yār Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْعَلَمَانِ ameandika katika ukurasa wa 629 ya Nūr-ul-‘Irfān, ‘Aya hii inabainisha kuwa ni bora kupumzika usiku na kujitafutia riziki wakati wa mchana. Usikae macho usiku ovyo wala kutumia mchana wako kwa mambo ya kipuuzi. Si makosa mtu kulala mchana na kufanya kazi usiku ikiwa ana dharura na kazi yake ni usiku.’

## Fadhila ya asubuhi

Unapopanga ratiba yako, fikiria vizuri kuhusu muda na aina ya kazi. Kwa mfano, ndugu waislamu wanaolala mapema, huamka asubuhi ili hali ni wakakamavu. Kwa hivyo majira ya asubuhi ni mazuri kwa shughuli za masomo. Du'a ifuatayo ya Mtume عَزَّوَجَلَّ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ imetajwa katika Tirmizi: 'Ewe Allah watilie baraka umma wangu katika asubuhi yao.'

*(Jāmi' Tirmizī, juz. 3, uk. 6, Ḥadithi 1216)*

Katika kusherehesha, Mufti Aḥmad Yār Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْمَعَانِ amesema, 'Maana yake, (Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ) Yabariki matendo yote ya umma wangu ya kidunia na kidini wanayoyafanya asubuhi. (mfano. safari, kutafuta elimu, biashara, nk).'

*(Mirāt-ul Manājīh, juz. 5, uk. 491)*

Panga shughuli zako za kila siku vizuri kuanzia unapoamka hadi unapolala. Kwa mfano, wakati fulani; Taḥajjud, shughuli za kimasomo, kusali sala ya Alfajiri (na sala zingine) msikitini kwa Takbira ya kwanza, sala ya Ishraki na Dhuha, kiamsha kinywa, mapato ya halali, chakula cha mchana, shughuli za nyumbani, shughuli za jioni, kuwa na watu wazuri (ikiwa hili haliwezekani, basi bora upweke) mkutano na ndugu waislamu kwa mas'ala ya kidini nk.

Shughuli zote hizi zipangiwe wakati maalum. Wale ambao hawakuzoea, mwanzo mwanzo watapata tabu lakini taratibu watazoea na wataona baraka, إِنْ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ.

Ndugu waislamu! Nikihitimisha bayana yangu, nitataja ubora wa kutenda sunna, na baadhi ya sunna na adabu. Amesema Mtume wa Rehema, Mtetezi wa ummah, Mmiliki wa Pepo صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ‘Anayependa sunna zangu ananipenda mimi na anayenipenda mimi atakuwa nami Peponi.’

*(Mishkāt-ul-Maṣābīh, juz. 1, uk. 55, Ḥadithi 175, Dār-ul-Kutub Ilmīyah, Beirut)*

## Maua 15 ya hekima kuhusu kulala na kuamka

1. Kukuta matandiko yako vizuri kabla ya kuyalalia ili kuondoa vidudu.
2. Soma du’a ifuatayo kabla ya kulala:

اللَّهُمَّ بِأَسْبِكَ أَمُوتُ وَأَحْيَا

**Tafsiri:** Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ Ninakufa na ninaishi kwa jina lako (ninalala na kuamka). *(Ṣaḥīḥ Bukhārī, juz. 4, uk. 196, Ḥadithi 6325)*

3. Usilale baada ya sala ya Alasiri kunaweza kusababisha wazimu. Amesema Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ‘Anayetelekeza akili yake kwa ajili ya kulala baada ya sala ya Alasiri hana wakumlaumu ila yeye mwenyewe.’

*(Musnad Abī Ya’lā, juz. 4, uk. 278, Ḥadithi 4897)*

4. Ni vizuri kupata lepe la usingizi majira ya saa nane. *(Fatāwā 'Alamgīrī, juz. 5, uk. 376)* Şadr-ush-Sharī'ah, Badr-ut-Tarīqah 'Allāmah Maulānā Muftī Muhammad Amjad 'Alī A'zamī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ameandika, 'Haya bila shaka ni kwa ajili ya wale ambao hukaa macho usiku wakifanya ibada kwa kumkumbuka Allah عَزَّوَجَلَّ au wakijitahidi kusoma. Mapumziko huondoa uchovu kwa ajili ya kukaa macho usiku.' *(Bahār-e-Sharī'at, juz. 16, uk. 79, Maktabah-tul-Madinah)*
5. Ni makruhu kulala mwanzo wa siku au kati ya sala ya Magharibi na Ishai. *(Fatāwā 'Alamgīrī, juz. 5, uk. 376)*
6. Ni bora kulala katika hali ya tohara.
7. Ni bora kulala kwa ubavu wa kulia na mkono wa kulia chini ya shavu la kulia kuelekea Qibla kwa muda halafu kulalia ubavu wa kushoto. *(Fatāwā 'Alamgīrī, juz. 5, uk. 376)*
8. Unapokwenda kulala, tafakari 'kulala' kaburini ambapo huna mshirika ila amali zako.
9. Unapokwenda kulala mkumbuke Allah عَزَّوَجَلَّ (sema, 'لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ' 'سُبْحَانَ اللَّهِ' an 'الْحَمْدُ لِلَّهِ') mpaka utakapolala kwani mtu ataamka katika hali ile ambayo alilala na atafufuliwa Siku ya Kiama katika hali ile ile aliyofia.

*(Fatāwā 'Alamgīrī, juz. 5, uk. 376)*

10. Baada ya kuamka soma du'a ifuatayo:

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَحْيَانَا بَعْدَ مَا أَمَاتَنَا وَإِلَيْهِ النُّشُورُ

Sifa njema zote ni za Allah عَزَّوَجَلَّ aliyetupa uhai baada ya kifo na tutaregea kwake.

*(Ṣaḥīḥ Bukhārī, juz. 4, uk. 196, Ḥadīthi 6325)*

11. Baada ya kuamka, tia nia ya kufanya amali njema na ujikinge kuudhi (watu) wengine. *(Fatāwā 'Alamgūrī, juz. 5, uk. 376)*

12. Msichana na mvulana wanapofikisha miaka 10, wasilale kitanda kimoja. Mvulana wa umri huu asilale na rika lake au wanaume (watu wazima) katika kitanda kimoja.

*(Dur-re-Mukhtār, juz. 9, uk. 629)*

13. Mume na mke wanapolala kitanda kimoja wasimruhusu mtoto wa miaka 10 kulala nao. Mvulana anapobaleghe, anahisabiwa kama mwanamume (mtu mzima).

*(Dur-re-Mukhtār, juz. 9, uk. 630)*

14. Tumia mswaki (kusafisha meno) unapoamka.

15. Ni ibada kubwa kuamka usiku kusali Tahajjud. Amesema Mtume wa Rehema, Mtetezi wa umma صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ,

‘Baada ya sala za faradhi hakuna sala yenye ubora kama ile sala inayosaliwa majira ya usiku.’

*(Ṣaḥīḥ Muslim, uk. 591, Ḥadīthi 1163)*

Kujifunza matendo kadhaa ya sunna nunua kitabu kinachoitwa ‘Sunnatayn aur Ādāb’ kutoka Maktaba-tul-Madīnah. Kusafiri na kundi la Madanī Qāfilahs la Dawat-e-Islami pamoja na wafuasi wa Mtume ni njia bora ya kujifunza na kutekeleza sunnah.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

### **Katika vinywaji baridi huwekwa gesi mbaya**

Katika vinywaji baridi huchanganywa na gesi mbaya aina ya karbond oxide ambayo husababisha chem chem ambayo hapana shaka huleta ladha lakini hiyo chem chem inatokana na gesi mbaya na yenye sumu ambayo tunaitoa sisi kutokana na pumzi yetu na kisha tunaipeleka kwenye mwili wetu kwa kufanya hivyo siyo uziri kabisa.

## Baraka Za Sunnah

Katika maringira mazuri ya Dawat-e-Islami (Shirika la Kimataifa la Kaeneza Mafundisho ya Quran na Surna liliojibusha na siana) sunna za Bwana Mtume **صلوات الله وسلامه عليه** zinafanana kwa wingi.

Ni ombi kwa kila muislamu kuhudhuria na kukesha usiku mzima kwa nia ya kutaka radhi za Allah **صلى الله عليه وسلم** pamoja na niya zingine nzuri katika ijimai ya kila wiki siku ya Alhamisi baada ya sala ya Magharibi inayofanyika katika mji anacishi. Vile vile ni ombi kwa kila muislamu kusafiri na wapenzi wa Mtume **صلوات الله وسلامه عليه** katika Madani Qafila kwa nia ya kupata thawabu na kujifunza sunna za Bwana Mtume **صلوات الله وسلامه عليه**. Na afanye Fikr-e-Madina (kujisili mwenyewe) kwa kujaza kadi ya Madani In'amaat na amkabidhi Zimmedaar (msimamizi) wake katika siku kumi za mwanzo za kila mwezi. Kwa Baraka ya kufanya hivyo **بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ** tutaweza kushikamana na sunnah za Mtume **صلوات الله وسلامه عليه** na tutachukia maasi na tutatiki kuwa na hamu ya kulinda imani yetu.

Kila muislamu aweke amna ya kwamba: "Nitajaribu kusubuhisha nafsi yangu na watu wote wa ulimwengu mzima" **بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ**

Kwa ajili ya kusubuhisha nafsi yangu nita fiuta Madani In'amaat na kusubuhisha nafsi za watu wa ulimwengu nita safiri katika Madani Qafila. **بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ**



ISBN 978-969-631-524-7



0109558



MC 1286

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran  
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan.

UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 1262

Web: [www.dawateislami.net](http://www.dawateislami.net) | E-mail: [translation@dawateislami.net](mailto:translation@dawateislami.net)